

Utabaini:

Mtu aliyepimwa chanya kwa COVID-19 ambaye hutangazwa tarehe 13 Machi kuhusu tawi la Manchester la Mgawanyiko/Idara la NH la Magari ya Motor [NH Division of Motor Vehicles] katika 377 South Willow Street ndani ya Manchester. Watu ambao walikuwa katika eneo la DMV la Manchester siku zifuatazo wanaweza kuwa walikuwa wazi/karibu na coronavirusi riwaya ambalo husababisha ugonjwa wa COVID-19 na ni lazima kufuatilia afya zao kwa homa au ugonjwa wa kupumua:

- Jumatatu, 2 Machi, kutoka saa mbili za asubuhi hadi saa kumi na nusu za jioni [8:00 am to 4:30 pm]
- Jumanne, Machi 3, kutoka saa mbili za asubuhi hadi saa kumi na nusu za jioni [8:00 am to 4:30 pm]
- Jumatano, Machi 4,
- Alhamisi, Machi 5, kutoka saa mbili za asubuhi hadi saa kumi na nusu za jioni [8:00 am to 4:30 pm]
- Jumanne, Machi 10, kutoka saa mbili za asubuhi hadi saa kumi na nusu za jioni [8:00 am to 4:30 pm]

Watu ambao walikuwa katika DMV ya Manchester siku yoyote ya hizo na kuwa na dalili za homa, kikohozi au upungufu wa pumzi lazima kukaa nyumbani, kupunguza mawasiliano yao na wengine, na mara moja kuwasiliana na mtoa huduma wao wa afya.

Watu ambao walikuwa katika DMV ya Manchester na hawajapata dalili lazima wajichunguze binafsi kwa dalili na kama wakipata/wakiona dalili wanapaswa kuwasiliana na mtoa huduma wa afya.

Tafadhali angalia **mwongozo wa kujichunguza binafsi** kwa msaada.
